



Lambeth Conference

Tangazo kwa Maaskofu wa Anglikana

Aprili 27, 2021

Safari ya kufika Lambeth Conference itanzia mtandaoni - Mfululizo wa Mazungumzo ya Maaskofu kwa njia ya mtandao yatafanywa mwaka 2021 - kwa ajili ya maandalizi ya Lambeth Conference mwaka 2022.



Lambeth Conference unapangwa kufanyika katika msimu wa kiangazi mwaka 2022. Mwaka 2021, kwa kujiandaa na tukio hilo, mfululizo wa vikao kwa njia ya mtandao kabla ya mkutano vitakuwepo kwa ajili ya Maaskofu wa Anglikana.

Kuanzia Julai 2021, 'Mazungumzo ya Maaskofu' yatawaalika Maaskofu wa Anglikana wakutane mtandaoni, ili waanza kuchunguza mada ya 'Kanisa la Mungu kwa ajili ya Ulimwengu wa Mungu'. Shughuli zaidi zimepangwa kwa ajili ya robo ya kwanza ya mwaka 2022. Maaskofu wanaalikwa kuhudhuria vikao sita, mara moja kwa mwezi.

Kwa kutafakari mada kutoka Petro 1, makundi yatajumuisha muda kwa ajili ya sala na kujifunza Biblia, kubadilishana uzoefu na visa kuhusu huduma na kujadili kuhusu kile kinachomaanisha Usharika wa Anglikana kushughulikia mahitaji ya ulimwengu unaobadilika haraka.

'Mazungumzo ya Maaskofu' yatasaidia kutambua vipaumbele na matumaini ya pamoja kabla ya mkutano wa ana kwa ana, na kuunda na kuimarisha mipango ya programu za mkutano.



Mikutano ya mtandaoni itahudhuriwa na maaskofu wote wanaofanya kazi katika Usharika wa Anglikana. Usajili kwa ajili ya vikao sasa umefunguliwa na maaskofu wanatumiwa barua pepe na kampuni inayoandaa mkutano huo ikiwa na maelezo yote ya usajili. Mikutano hii ni ya hiari.

Mikutano hii inaandaliwa na Kundi Linalofanya Kazi la Lambeth Conference, Mwenyekiti akiwa ni Askofu Emma Ineson. Watasaidiwa na timu ya Maaskofu waandaaji na wawezeshaji inayoundwa na watu anuwai na wenye vipaji kutoka katika Ushirika wote wa Anglikana ili kufanikisha vikao hivi.

Askofu Emma alisema: *Lambeth Conference hutoa fursa ya mara moja baada ya miaka kumi kwa maaskofu wa Anglikana ulimwenguni kote kukutana pamoja kwa ajili ya sala, ushirika na mazungumzo. Kwa kuwa sasa mkutano utafanyika mwaka 2022, kukutana mtandaoni kabla ya mkutano hutoa fursa maalumu kwa ajili ya maaskofu kuanza kujiandaa, kukutana na kujadili mada za mkutano. Tunajua kwamba maisha ya askofu yametingwa na shughuli nyingi, lakini tunatumaini kwamba maaskofu watatumia fursa ya kushiriki kwenye mazungumzo ya kabla ya tukio. '*

Phil George, Mkurugenzi Mtendaji wa Lambeth Conference alisema: *Usharika wa Anglikana unaundwa na watu anuwai wanaozungumza lugha mbalimbali. Timu ya mkutano inafanya kazi kwa bidii kuunda makundi ambayo yanawasaidia maaskofu kutoka katika majimbo mbalimbali wakutane pamoja, kuhudumia tofauti za majira katika maeneo mbalimbali na kuzingatia huduma za lugha/ukalimani. Tunatazamia kwa shauku kubwa kuona Mazungumzo ya Maaskofu kabla ya tukio yakifanyika.*

Unaweza kushiriki vipi?

Ratiba ya Mazungumzo ya Maaskofu na maelezo zaidi hupatikana kwenye tovuti ya Lambeth Conference.

Itazame hapa: <https://www.lambethconference.org/programme/bishops-conversations/>

Mazungumzo ya Maaskofu ni kwa ajili ya Maaskofu wote wa Anglikana katika Usharika wa Anglikana.

Maaskofu watakuwa wamepokea maelezo ya usajili kupitia barua pepe kutoka timu ya usajili wa matukio ya Lambeth Conference. Maaskofu wanapaswa kuangalia barua pepe zao kwa ajili ya mawasiliano haya.

Ikiwa hujapokea maelezo, au ungependa maelezo hayo yatumwe tena, tafadhali tuma barua pepe kwenda Timu ya Lambeth Conference kupitia:

info@lambethconference.org